*AAP 72 (2002) • SWAHILI FORUM IX • 19–24*

# SUFII AL-BUSIRI

KINEENE WA MUTISO

## 1. Utangulizi

Katika makala hii nitazungumzia tarehe na kazi za al-Busiri mshairi wa kisufii maarufu katika fasihi ya kiislamu na ambaye baadhi ya kazi zake zimetarjumiwa kwa Kiswahili. Mojawapo ya kazi hizi ni ***Kasida ya Hamziyyah,*** ambayo ni maarufu sana hususa kwa Kiswahili cha zamani kiitwacho Kingozi. Kazi yake ya pili mashuhuri sana *ni* ***Kasida ya Burudai,*** kasida ambayo ndiyo maarufu zaidi katika ulimwengu wa kiislamu. Mshairi huyu ingawa ni mashuhuri, ni mgeni sana kwa wasomi wengi wa fasihi ya Kiswahili.

### 1.1. Sufii Sharafu d'-Dini Muhammad bin Sa'idi bin Hammadi bin Muhsini bin Sanhaji Hilali as-Sanhaji al-Busiri (1213-1294): Historia yake fupi

Sharafu 'd-Dini Muhammad bin Sa`idi bin Hammadi bin Muhsini bin Sanhaji Hilali as-Sanhaji **al-Busiri** anajulikana kama Muhammad ibn Saeed ibn Hammad, Sharfuddin Abi Abdullah al-Busairi, Sharaf ad-Din Abu `Abd' Allah Muhammad B. Said B. Hammad al-Misree, Abu `Abdi 'Allah Muhammad B. Said, Sharaf ad-Din Muhammad Said B. Hammad B. Muhsin al-Buswairy, Sharafu 'd-Dini Abu Abdallah bin Muhammad bin Said 'd-Dilasi al-Busiri as-Sanhaji, na Sharafu 'd-Dini Muhammad bin Said bin Muhsini bin Sanhaji Hilali as-Sanhaji al-Busiri alizaliwa katika kijiji cha Dalas, Moroko, katika mwaka wa 608 A. H./1212 B. K., akakulia al-Busiri, Misri, na kufia huko Alexandria mwaka wa 694 A. H./1294 B. K.

Alikuwa ni mshairi wa kimisri mwenye asili ya kabila la kiberber, la huko Moroko, na alizaliwa tarehe 1 Shawwal 608 H/Marchi 7th, 1213 BK, huko Busir (Abusir) au karibu na Dalas (Dilas), Misri ya Juu. Wazazi wake walihamia Misri kutoka Moroko. Alikulia katika mji wa Busir na ndio sababu akapatiwa jina la kupanga au la watani (Kiarabu, **nisba***),* **al-Busir**. Aidha alijulikana kwa jina lingine la watani wa Dalas (Dilasi). Inasemekana kwamba mmoja wa wazazi wake alitoka Dalas na ndio sababu mshairi huyu akaitwa **Dalasir/Dalasir**. Jina lile lingine lake la lakabu lilikuwa ni Shariffud-Din (Kutukuzwa kidini).

Katika ujana wake alisoma kwa kiasi katika msikiti wa Sheikh Dhahir, huko Kairo (Cairo). Alijifundisha usufii, fasihi ya Kiislamu, kunga za lugha ya Kiarabu, kukariri ***Qurani Takatifu*** kwa moyo, historia ya Usilamu, Hadithi na sira ya mtume Muhammadi, kunukuu miswada, uchoraji na utiaji wa nakshi. Sheikh wake alikuwa ni Sheikh Abu 'l 'Abbas Ahmad al-Mursi, ambaye alikuwa ni Sufii mashuhuri. Wazazi wake walikuwa maskini na kwa sababu hii

alianza kutafuta kazi akiwa mdogo. Alijipatia pesa kutokana na kazi yake ya kutia nakshi (kaligrafia). Usufi na kaligrafia zilikuwa ni kazi zilizonasibishwa na usomi siku hizo.

Baadaye alikwenda Bilbis na kujipatia kazi ya uhasibu. Huko Bilbis alijulikana kwa kupenda kubishana na wafanyi kazi wenzake wa Kikristo na wa Kiyahudi kuhusu ***Biblia Takatifu*** na ***Taurati***. Alisoma dini ya kiyahudi (Ujuda) na ya Ukristo, ili aweze kujitetea vizuri katika mijadala mikali baina yake na Mayahudi na Wakristo.

Ingawa hakusoma sana alibahatika kupata kazi ya ualimu. Aidha aliwatukuza viongozi na matajiri wa nchi yake kwa ushairi wake na nia kubwa yake ilikuwa ni kujipatia riziki na sifa. Inasemekana ya kwamba alipenda kuwategemea watu sana na hakutosheka na kazi alizofanya. Aidha inasemekana ya kwamba al-Busiri, ambaye alikuwa mtu mfupi na kimbaombao, alikuwa mara kwa mara akifanyiwa stihizai na watu. Naye alikuwa akipandwa na mori kwa haraka na kuwatukana kwa lugha chafu sana. Watu wengi hawakumpenda al-Busiri, kwa sababu ya matusi yake.

Ni maskini ambaye, yasemekana, hakupenda kuwa mzazi, alijuta kuoa, alitamani kutokuwa na watoto, alitamani mkewe awe tasa, alitamani kuwa mtumishi wa mtu mwingine kuliko kuwa baba na alitamani kuwa shoga kama baadhi ya masufii wa siku hizo. al-Busiri hakupenda kutulia mahali pamoja kwa muda mrefu. Alitanga karibu Misri nzima akiwasifu matajiri wa huko. Inaaminika ya kwamba alimsifu meya wa al-Mahala, mji uliokuwa kusini mwa mashariki ya Kairo naye akawa akimlipa mshahara wa mwezi. Huyo meya alipoucheleweshaa mshahara wake, al-Busiri alikuwa akimghadhibikia na kuwatusi Wakristo waliofanya kazi katika ofisi yake. Baadaye alihama mahali hapo (al-Mahala) lakini hakuwasamehe Wakristo wa hapo. Jambo hili lajitokeza katika ushairi wake, hususa katika ***Hamziyah***.

Alihudhuria hotuba za Shadhili Sufi Shaikh Abu 'Abbas Ahmed al-Mursi (al-Marsi) aliyekufa hapo 684 H/1287 BK. al-Marsi mwenyewe alikuwa ni Sufi na ni wazi kwamba alimwadhiri sana al-Busiri. Kama Sufi, al-Busiri alihusika katika ukuzaji wa Shaddhiliya. Kikundi hiki cha masufii kilihusika na usambazaji wa kasida moja maarufu ya al-Busiri ijulikanayo kama ***Burdat al-madih***. Huko Kairo, katika msikiti wa Sheikh Abdal Dahir, alisomea sayansi ya Uislamu, lugha, ismu na fasihi ya Kiarabu. Kama Sayyid Aidarusi alisomea sheria za kiislamu, historia na maendeleo ya Uislamu, ufafanuzi na ukariri wa ***Kur'ani Tukufu***, Hadith, na Usufi.

al-Mursi, mkufunzi wa kisufi wa al-Busiri, alikuwa akisifika huko Aleksandira kwa kuifasiri ***Kur'ani Tukufu***. Alipotimia miaka kumi na mitatu, al-Busiri aliweza kuikumbuka ***Kur'ani Tukufu*** yote. Alikuwa mjuzi wa ***Kur'ani Tukufu*** pamoja na Hadith. Wa aidha likuwa ni Sufi alizeelimika.

al-Busiri alikuwa na hamu na hamumu ya kuizisoma lugha za kimashariki. Hata hivyo, hakuwa amesoma sana, kulingana na elimu ya siku hizo. Hakuwa mwalimu, kazi iliyokuwa ya

mtu aliyesoma sana wakati huo. Maadam familia yake ilikuwa masikini, alilazimika kujitafutia riziki yake akiwa mdogo. Alijipatia riziki yake kwa kufanya kazi ya utiaji wa nakshi.

Hata hivyo, umaarufu wake hautokani sana na ujuzi wake wa kaligrafia bali na baadhi ya kasida zake alizotunga kumsifu Mtume Muhammad. Kwa miaka kumi aliishi Mukaddasi (Yerusalemu) halafu Makkah na baadaye Madinah, ambako ndiko alikotungia ***al-Burdah*** (***Kasida ya al-Burdah***) ile kasida maarufu, ambayo imetafisiriwa kwa Kiswahili na maudhui yake ni sehemu ya maudhui ya ***Kasida ya Hamziyyah***. Baadaye alihamia Madinah na kisha kuishi huko Bilbis.

Huko Bilbis alikuwa na kazi ndogo ya uhasibu, katika afisi ya waziri wa kimamluk, Zainuddin Yaqub bin Zubair, waziri wa korti. Waziri huyu alikifahamu kipawa cha utunzi cha al-Busiri na alimshauri atunge mashairi ambayo kwayo mara kwa mara alimtuza zawadi nono. Alikuwa ni kama mlezi wa al-Busiri katika utunzi wake.

Ni huko Bilbis ambako, kwa mara ya kwanza, al-Busiri alijipatia riziki yake kwa utunzi na kwa kaligrafia. Kwa muda mfupi alipanda cheo na kuwa mshairi wa mahakama. Huko Bilbis, alikuwa akiwa akibishana na wafanyi kazi wenzake, wa Kinasara na Kiyahudi, juu ya ***Taurati***, ***Kur'ani Tukufu*** na ***Biblia Takatifu***. Mabishano hayo yalimfanya avutiwe na kuusoma zaidi Ukristo na Uislamu.

Al-Busiri alikuwa ni mtu mfupi na mwembamba, ambaye watu walimfanyia mzaha. Kwa upande wake naye aliwashambulia kwa kuwatusi vibaya sana. Watu wengi walimchukia kwa sababu ya kiburi na matusi yake mabaya.

Katika ushairi wake aliwatukuza matajiri na wenye mamlaka katika nchi yake. Hivi ndivyo alivyojipatia riziki na umaarufu wake. Alijulikana kama mwenye kupenda kuwategemea watu wengine ili waweze kumfadhili. Alichukia kuwa mume. Alisikitika kuoa na kuwa na watoto. Alitamani mkewe awe tasa. Aidha alitamani kuwa mfanyikazi wa mtu kuliko kuwa baba watoto. Hata alitamani kuwa basha, kama masufi wenngi wa siku hizo (Kilani 1973: 22).

Hakuisha mahali pamoja kwa muda mrefu bali alizurura Misri nzima akiwasifu matajiri kwa ushairi wake. Mathalani, alimsifu meya wa al-Mahala, mji uliokuwa Kusini Mashariki mwa Misri. Huyu meya alimlipa mshahara kila mwisho wa mwezi.

Mara kwa mara alikuwa akikasirishwa na meya, alipomcheleweshea mshahara wake. Aliwachukia Wakristo wa al-Mahala, ambao walifanya kazi katika afisi ya meya. Hata baada ya kutoka al-Mahala, al-Busiri hakuwasamehe hao Wakristo, ambao walikuwa ni wafanyikazi wenzake. Katika ***Kasida ya Hamziyyah***, tunaona vile al-Busiri anavyowashambulia vikali Wakristo na Mayahudi.

Alipozeeka, al-Busiri aliutumia muda mwingi wake katika kumtumikia Mwenyezi Mungu katika dini ya Kiislamu. Alikuwa akiwasiliana na Abdal-Salam bin Mashish al-Husun, kiongozi wa Kiisalmu, kama yule shehe wake - Abul `Abbas Ahmad al-Mursi al-Ansari.

Ingawa alitunga mashairi mengi, ni kasida za kumsifu Mtume Muhammad ambazo zinasifika zaidi, katika upande maudhui na ujumi. Maaudhui katika mashairi yake yahusu wasifu, tashtiti, majibu yake kwa Manasara na Mayahudi na pia ucheshi. Aliyatunga mashairi kutokana na mapenzi na mapendekezo ya Zainuddin Yaqoob bin Zubair.

Akimdondoa ibn Hajr al-Haythami, Lubis ((1983: 10) anasema kwamba umaarufu wa al-Busiri watokana na sio ushairi tu bali pia tutumbi. Hata hivyo, Muhammad Sayyid Kilani (1973) anayapinga maoni haya. Yeye anasema ya kwamba tutumbi ya pekee aliyoitunga al-Busiri ni ni sherehe ya shairi lake lijulikanalo kama ***al-Makhraj wa al-Mardud `ala al-Nasara wa Yahudi.*** Tutumbi hii, kulingana na Muhammad Sayyid Kilani, haionyeshi ustadi wa al-Busiri katika uandishi wake.

Katika toleo la kwanza la ***Encyclopaedia of Islam Vol.I*** (1911-38:252, 804) kuna makala ya hayati René Basset juu ya al-Busiri. Katika makala haya, René Basset anadai ya kwamba kaburi la al-Busiri liko karibu na lile la Imam as-Shafii, huko Kairo. Maoni kama hayo yametolewa katika ***Dairat al-Ma `arif al-Islamiyya*** *Vol IV* (1933:329) na tena katika ***Urdu Da'ira-i Ma'arif-i Islamiyya Vol.V*** (1971:52). Carl Brockelmann katika *Geschichte der arabischen Litteratur* anadai ya kwamba al-Busiri alifia huko Alexandria lakini alizikwa katika makaburi ya kusini, Kairo, karibu na kaburi la Imâm al-Shâfi`î. Maoni kama haya pia yanapatikan katika fasihi ya Kiarabu ya karne ya kumi na saba lakini ni maoni ya kupotosha, ambayo yanatokana na maoni yaliyotolewa na Louis Massignon, ambaye aliandika kuhusu makaburi ya Kairo.

Katika utafiti wangu huko Kairo na Aleksandria, Misri, niliweza kudhibitisha ya kwamba kaburi la al-Busiri liko Aleksandria na wala sio Kairo, kinyume na madai kwamba liko karibu lile la Imam as-Shafii, kama ambavyo imedaiwa katika ***Encyclopaedia of Islam*** (1911-38:108) au anavyodai Jan Knappert (1971b:167). Al-Busiri alifia huko Alexandria na kaburi lake ni mashuhuri na hutembelewa na mahujaji.

Wataalamu wengine hawatofautishi Abul Qasim Hibat Allah bin Ali bin Masud al-Ansari al-Khazraji al-Munastiri (aliyekufa 1201BK) na al-Busiri. Abul Qasim Hibat Allah bin Ali bin Masud al-Ansari al-Khazraji al-Munastiri pia hujulikana kama al-Busiri na ni ulema maarufu zaidi ya al-Busiri. Al-Khazraji anaitwa al-Busiri kwa sababu babu yake, Masud alihama kutoka Munastiri hadi Busir Quridis.

Hata Sa`adat Ali Basha Mubarak (1886-88:70), ameeleza ya kwamba kaburi la al-Busiri liko Alexandria na hayati Said Basha alikarabati Masjid al-Busiri na kutoa pesa za kuendesha shughuli kam vile mihadhara ya kidini. Aidha Zaki Mubarak (1926:164, 1935b:141)anadhibitisha kwamba kaburi la al-Busiri liko Alexandria na kwamba kaburi hili pia kwenye kaburi hili kuna msikiti, ambamo huwa na mihadhara ya kidini.

Kati ya Aleksandria ya zamani, karibu na msikiti wa Abû l-`Abbâs al-Mursî al-Shâdhilî (mwanafunzi wa sufi Abû l-Hasan al-Shâdhilî) na kusini mwa misikiti mikubwa ya sehemu

hiyo, kuna msikiti na pia kaburi la al-Bûsîrî. Msikiti huu na kaburi lake hususa hutembelewa na wanawake wanaowabeba watoto wadogo wao, kwa sababu ya baraka za mahali hapo.

### 1.2. Kazi za al-Busiri

Kazi za al-Busiri zaweza kugawanywa katika vipindi viwili: Zile alizozitunnga kabla na kuhiji na zile alizozitunga baada ya kuhiji.

#### 1.2.1 Kazi alizozitunga kabla kuhiji

Baadhi ya zile alizitunga kabla ya ya kuhiji ni: al-Qasidah al-Lamiyah, al-Qasidah al-Haiyah, al-Qasidah al-Daliyah na al-Qasidah al-Mimiyah. Kazi zile alizitunga baada ya kuhiji ni: al-Qasidah al-Hamziyyah (Umm al-Qura fi Madh Khayr al-Wara), al-Qasidah al-Baiyah na al-Qasidah al-Mimiyah (al-Kawakib al-Durriyah fi Madh Khayr al-Bariya au al-Burdah). al-Qasidah Hamziyyah pia inajulikana kama Hamziya fi'l Madaih li-Nabawiya.

Kazi zingine zake ni kama vile Dhukhr al-Ma`ad 'ala wazn Banat Su`ad (katika kazi hii anamwiga Ka`b bin Zuhair katika kasida yake maarufu ijulikanayo kama, Banat Su`ad), al-Qasidah al-Khamriya, al-Qasida al-Mudariyya fi'l-salat 'ala Khayr al-Bariyya, al-Qasidah Ya'iyya na al-Tawassul bi 'l-Kur'an.

Kasida ya Burudai ni kazi ya al-Busiri ambayo imetarjumiwa katika lugha si haba za ulimwengu.

#### 1.2.2 Kasida ya Burudai

Maudhui yote yaliyo katika kasida hii yapatikana katika ***Kasida ya Hamziyyah***. Ni sehemu ya maudhui ya ***Kasida ya Hamziyyah,*** maadamu kuna maudhui ambayo yako katika ya ***Kasida ya Hamziyyah*** ambayo hayapatikani katika ***Kasida ya Burudai***.

***Burudai*** au ***Qasidatu 'l-Burda*** ni kasida ambayo inamtukuza Mtume Muhammadi na inasifika sana kwa vile inasemekana ya kwamba beti zake zina nguvu za kiajabu. Kasida hii huimbiwa au kukaririwa mgojwa mahtuti. Inasemekana, pia, ya kwamba kasida hii hukaririwa kwenye matanga na kwamba hakuna shairi lingine la Kiarabu ambalo limewahi kupata sifa kama hizi. Kuna fasiri zaidi ya tisini ambazo zimeandikwa kuhusu kasida hii, kwa lugha za Kiarabu, Kifursi (Kiajemi), Kiturki na Kiberber.

Kazi hii pia imetungwa kwa bahari si haba za aina ya ***tathlith, tashtir*** na ***takhmis***. Kasida yenyewe inaanza kwa mtindo wa ***nasib,*** mtindo ulio maarufu sana katika ushairi wa Kiarabu, halafu mshairi anasikitikia maisha ya ujana wake na kutubu dhambi zake. Mshairi anayatofautisha matendo yake na yale ya Mtume ambaye sifa zake anazichora kwa ustadi sana.

**Marejeleo**

*Encyclopaedia of Islam*. 1913-1936. Vol. I - Vol. IV (1965-1979). Leiden: E. J. Brill.

Kilani, Mohammed Said. 1973. *Diwani al-Busiri*. Cairo: Mustafa al-Babi al-Halabi and Sons Publishing Company.

Knappert, Jan. 1971b. *Swahili Islamic Poetry Vol. II: The Two Burdas*. Leiden: E. J. Brill.

Lubis, Haji M.Bukhari. 1983. *Qasidah's in honor of the Prophet*: A Comparative study between al-Busiri al-Burdah and 'Attar's N'at in his Illahi-Namah, Penerbit University Kebangsan, Selangor, Malaysia.

Mubarak, Zaki. 1935a. *Anasir al-Burda in Madaih an-Naba-wiyah fi al- Adab al-Arabi*, Matiba'ah Mustafa al-Babi, Al-Halabi wa Awala-dih, al-Qahirah.

Mubarak, Zaki. 1935b. *al-Madai & al-Nabawiyah fi al-Adab al-Arabi*. Cairo: Dar al Katib al 'Arabi.

wa Mutiso, Kineene. 1985. *Hurafa na Uyakinifu katika Hamziyyah* (tasnifu ya M.A.ambayo haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

wa Mutiso, Kineene. 1996. *Archetypal Motifs in Swahili Islamic Poetry: Kasida ya Burudai* (tasnifu ya Ph.D. ambayo haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.